

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII  
IDARA YA WANYAMAPORI  
TAASISI YA TAALUMA YA WANYAMAPORI**



**TUNAPENDA KUTOA TAARIFA KWA WAOMBAJI WOTE AMBAO  
HAWAJACHAGULIWA KUJIUNGA NA MASOMO MWAKA 2016/2017 KAMA  
IFUATAVYO;**

**1. WENYE CHETI CHA MAFUNZO YA MIEZI MITATU (3) (BASICS OF  
SHORT COURSE IN WILDLIFE MANAGEMENT AND LAW  
ENFORCEMENT)**

- i. Cheti cha kumaliza kidato cha nne (4) (form IV Secondary Certificate) hakina ufaulu wa masomo matatu kuanzia ufaulu wa D na kuendelea.
- ii. Kutokuwasilisha maombi kuonesha kwamba ana nia ya kuendelea na masomo kwa wakati.
- iii. Kutokumaliza ada ya mafunzo ya kozi fupi.
- iv. Vyeti vya kumaliza kidato cha nne kuwa na taarifa ambazo siyo sahihi . Ukiingiza katika mfumo wa udahili wa NACTE (Central Admission System-CAS) zinaleta jina ambalo siyo la kwake.

**2. WALIOMALIZA KIDATO CHA NNE (FORM IV) NA WALIOMBA KUSOMA  
'BASIC TECHNICIAN CERTIFICATE IN WILDIFE MANAGEMENT AND  
LAW ENFORCEMENT-(BTCWLE)**

- i. Ufaulu wa usaili kuanzia 50% kwa wasichana na 59% kwa wavulana.
- ii. Waombaji kuomba chuo zaidi ya kimoja, hivyo wakati wa kuingiza namba ya cheti chake cha kidato cha nne inaonesha kuwa amechaguliwa chuo kingine na hivyo system kumkataa.
- iii. Taarifa ya cheti cha kidato cha nne (index number) kuwa siyo sahihi.
- iv. Ufaulu wa masomo manne katika 'single examination sitting'

- 3. KWA WALIOSOMA ‘BASIC CERTIFICATE IN WILDLIFE MANAGEMENT AND LAW ENFORCEMENT’ (BTCWLE) KUOMBA KUSOMA ‘TECHNICIAN CERTIFICATE IN WILDLIFE MANAGEMENT AND LAW ENFORCEMENT’ (TCWLE)**
- i. Ufaulu wa chini ya masomo matatu (3) kwa kidato cha nne (form IV). Mfano wengi wana D mbili katika cheti cha kidato cha nne.
  - ii. Taarifa zinaonesha ameomba na amechaguliwa kujiunga na chuo kingine.
- 4. KWA WALIOSOMA KIDATO CHA IV NA WAMEOMBA KUSOMA TECHNICIAN CERTIFICATE IN WILDLIFE MANAGEMENT AND LAW ENFORCEMENT**
- i. Lazima awe amesoma kozi ya ‘Basic Technician Certificate in Wildlife Management and Law Enforcement au
  - ii. Awe amemaliza kidato cha sita na kufaulu kuwa na ‘principal and subsidiary’ moja .

IMETOLEWA;

**MKUU WA TAASISI**

9 AGOSTI, 2016